JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI NKOMOLO

S.L.P 36

NAMANYERE

TAREHE...../...../.....

Jina la Mwanafunzi.....

.....

KIJIJI/MTAA.....

MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NKOMOLO

1.0 UTANGULIZI.

Ninayo furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule hii mwaka **2021**. Shule ya sekondari Nkomolo ipo katika Mtaa wa mjimwema kata ya Nkomolo wilaya ya Nkasi mkoa wa Rukwa.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021**, Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021**, hivyo baada ya siku saba(**7**) unatakiwa uwe umeripoti shuleni vinginevyo nafasi yako itachukuliwa na mwanafunzi wa akiba.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

A. SARE YA SHULE

i/ WAVULANA:

Suruali:Anatakiwa awe na suruali mbili bluu bahari na kijani jeshi. Mshono wa suruali: iwe na mifuko mitatu mmoja nyuma upande wa kulia na miwili mbele pande zote kulia na kushoto pembeni na sio kubandika, iwe na rinda mbili kila upande na upindo wa chini (miguuni) ugeuzwe juu (turnup). Upana miguuni uwe wa kutosha isiwe ya kubana. Suruali za mitumba na jinsi haziruhusiwi hapa shuleni.

Shati:Awe na mashati mawili meupe(white) yenye mikono mifupi (short sleeve)

Viatu:Awe na viatu vyeusi vya ngozi vya kufungwa na kamba, na soksi rangi nyeupe, visiwe na sori ndefu na visivyo chongoka mbele.

Sweta:Awe na sweta rangi ya damu ya mzee yenye shingo "V" kwa ajili ya kujikinga na baridi.

Sare za michezo:Awe na physical Training short(P.T.Short) au Tracksuit rangi nyeusi na raba za michezo.

Nywele:Nywele ziwe fupi zenye kulingana muda wote.

ii/ WASICHANA:

Sketi:Anatakiwa awe na sketi mbili (2) bluu bahari na kijani jeshi, mshono wa sketi ziwe na rindabox kubwa moja mbele na moja nyuma na pembeni rinda mbili ndogo. NB: Sketi ziwe ndefu zifike kwenye viatu, sketi fupi haziitajiki. Hivyo mzazi unatakiwa kumshonea binti sketi ndefu ili kuepuka usumbufu unaojitokeza.

Shati:Awe na mashati mawili meupe(white) yenye mikono mifupi (short sleeves).

Viatu:Awe na viatu vyeusi vya ngozi vya kufungwa na kamba na soksi nyeupe, visiwe na sori ndefu na visivyo chongoka mbele.

Sweta:Awe na sweta rangi ya damu ya mzee lenye shingo ya "V" kwa ajili ya kujikinga na baridi.

Sare ya michezo:Awe na tracksuit rangi nyeusi na raba kwa ajili ya michezo.

Scanned with CamScanner

Nywele:Nywele ziwe fupi zinazolingana muda wote, hakuna kusuka wala kuweka dawa nywele.

B. VIFAA VYA MASOMO:

1. Daftari kubwa zisizopungua 10 (counterbook)
2. Mathematical set (mkebe) 1
3. Aje na kamusi moja ya kiingereza (Dictionary)
4. Aje na kalamu za kutosha,rula na penseli

C. CHAKULA CHA WANAFUNZI

Kutokana na maazimio ya kikao cha wazazi cha tarehe 06/12/2019 ni kwamba wanafunzi wote wanatakiwa kula chakula hapa shuleni. kwa wale wenye utayari wataanza kuchangia mwanzoni mwa mwaka kwa mchanganuo ufuatao:- **MILO MITATU KUTWA NA HOSTELI**

SN	CHAKULA/FEDHA	MWAKA MZIMA	NUSU MWAKA	ROBO MWAKA YA KWANZA JAN-APRIL 2021
1	MAHINDI	DEBE 10	DEBE 5	DEBE 3
2	MAHARAGE	DEBE 3	DEBE 1 NA NUSU	DEBE 1
3	SUKARI	KG 8	KG 4	KG 2
4	FEDHA	TSHS 60,000/=	TSHS 30,000/=	TSHS 15000/=

WANAFUNZI WA KUTWA KWA MILO MIWILI

SN	CHAKULA/FEDHA	MWAKA MZIMA	NUSU MWAKA	ROBO MWAKA YA KWANZA JAN-APRIL 2021
1	MAHINDI	DEBE 6	DEBE 3	DEBE 2
2	MAHARAGE	SADO 7	SADO 3 NA NUSU	SADO 2
3	SUKARI	KG 8	KG 4	KG 2
4	FEDHA	40,000/=	20,000/=	10,000/=

HOSTELI

Nafasi za hosteli zipo kwa wasichana tu ambazo ni chache sana, watakao hitaji kukaa hosteli mahitaji ni kama ifuatavyo

(i)Mahindi debe 10 kwa mwaka
(ii)maharage debe 3 kwa mwaka Na sukari kg 8 kwa mwaka
(iii)fedha TSH 60,000/= kwa mwaka ya mpishi, kuni, chumvi,mafuta ya kula na kusaga.
(iv)shamba dress rangi ya bluu (kitambaa cha satini)
(v)mashuka mawili rangi ya bluu 1 na pinki 1
(vi)chandarua
(vii)Ndoo mbili ndogo
(vii)Dumu tupu la lita tano kwa ajili ya kuhifadhia maji yake ya kunywa.
(viii)Sanduku la bati (tranka)
(ix)Tochi ndogo (kwa dharula mbalimbali)
(x)Vyombo vya chakula (sahani 1,kikombe 1, kijiko 1)

NB: Mzazi atakaye leta chakula kibovu (kilichopecha) hakitapokelewa. Pia mwanafunzi wa hosteli haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani na vyakula binafsi

3.0 Sheria na kanuni Muhimu za shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu **Na.25** ya mwaka **1978** na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria **Na.10** ya mwaka **1995.**

Scanned with CamScanner

Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu Nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi,wazazi, wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii yote kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote, na
(i) Kutunza mali ya umma.

3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kusimamishwa au kufukuzwa shule.

(i) Wizi

(ii) kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro

(iii) kugoma na kuhamasisha mgomo

(iv) kutoa lugha chafu kwa mwanafunzi mwenzako, mwalimu,mlezi na jamii nzima kwa ujumla.

(v) kupigana na mwanafunzi mwenzio, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule.

(vi) kusuka mtindo usiotakiwa, wanafunzi wanatakiwa kuwa na nywele fupi muda wote wawapo shuleni.

(vii) kufuga ndevu

(viii) ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevywa.

(ix) uvutaji wa sigara.

(x) uasherati, mausiano ya jinsia moja, kuoa au kuolewa.

(xi) kupata ujauzito au kutoa Mimba.

(xii) kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za Nchi.

(xiii) kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.

(xiv) kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.

(xv) kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

(xvi) kudharau bendera ya Taifa.

(xvii) kufanya jaribio lolote lile la kujiua,au kutishia kujiua kama vile kunywa sumu nk.

(xviii) uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

NB: Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu PIA AJE NA CHETI CHAKE CHA KUZALIWA NI MUHIMU SANA.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....

THE HEADMASTER
NKOMOLO SECONDARY SCHOOL
NKASI - RUKWA.

THOMAS L.MPANDASHALO
MKUU WA SHULE
0757635500/0627345194

Scanned with CamScanner

MEDICAL OFFICER

.....

.....

RE: MEDICAL EXAMINATION:

MR/MISS:.....

Please examine the above named student as to his/her physical and mental fitness for a full time student in this school. The examination should include the following categories.

1. Hemoglobin.....
2. P.v. Bleeding.....
3. Sight .....
4. Blood pressure.....
5. Urine for Sugar and pregnancy.....
6. Stool for routine examination.....
7. Asthma .....
8. Skin diseases.....
9. Leprosy.....
10. Pulmonary tuberculosis.....
11. Neurosis.....
12. Venereal diseases.....
13. Other serious diseases.....

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government Medical officer)

1. I have examined the above named student and consider that He/She is physically fit/ Unfit and mentally fit/ Unfit and mentally fit/ unfit for a full schooling.
2. Other comments.....
   .....
   .....

.....

SIGNATURE AND OFFICIAL STAMP

DATE .....

NB: ***NENDA HOSPITALI NA FOMU HII KWA AJILI YA VIPIMO KISHA IRUDISHE SHULENI.***

Scanned with CamScanner